

Sote tuna maswali mazuri kuhusu chanjo



Je, chanjo ya COVID-19...

Ni bila malipo? **NDIYO**

- Hakuna ada ili kupata chanjo.
- Ikiwa utatozwa ada ya kuweka miadi au kupata chanjo, ni ulaghai.

Ni ya watu wote? **NDIYO**

- Si lazima uwe na kadi ya RAMQ wala bima ya afya.
- Jina na tarehe yako ya kuzaliwa tu ndivyo utakavyoombwa.

Ni lazima? **HAPANA**

- Chanjo inapendekezwa sana kwa watu wote walio na zaidi ya miaka 16 (umri wa chini unaweza kubadilika kulingana na tafiti za sasa).

Ninaweza kukosa zamu yangu ya kupata chanjo?

HAPANA

Wakati wa zamu ya rika lako kupata chanjo, unaweza kuweka miadi. Unastahiki kupokea chanjo kuanzia tarehe hiyo na bado unaweza kupata chanjo baadaye, bila kujali wakati unapochagua kupata chanjo.

Chanjo ya COVID-19...

Itanipa COVID-19? **HAPANA**

- Chanjo zilizoidhinishwa nchini Kanada hazina virusi hai, hivyo haiwezekani kupata ugonjwa kupitia chanjo.

Inafanya kipimo cha COVID-19 kuwa na maambukizi? **HAPANA**

- Kipimo cha COVID kinachunguza tu ikiwa mtu ameambukizwa na anagua kutokana na virusi.

Ina bidhaa za mnyama au binadamu zenye sumu? **HAPANA**

- Hakuna chanjo iliyo na bidhaa za damu, zebaki, alumini, formaldehyde, seli za kiinitete, au bidhaa nyingine yoyote ya wanyama.

Nitakuwa kwenye hatari nikitaka kupata mtoto? **HAPANA**

- Hakuna ushahidi wa madhara ya matumizi ya chanjo za COVID kwenye uwezo wa kuzaa au kutozaa, yaani, chanjo haziathiri uwezo wa kuwa mjamzito wala wa kubeba ujauzito.
- Chanjo inaweza kupendekezwa kwa mtu mjamzito au anayenyonyesha ili kupunguza hatari ya COVID-19 na kuwa na kinga bora. Wasiliana na daktari wako.

Inaruhusu kufuatilia? **HAPANA**

- Chanjo hazileti maikrochipu kwenye mili yetu. Tunapopata moja ya chanjo za COVID-19, maelezo yetu binafsi hayashirikiwi na hatufuatiliwi. Chanjo ina vitu tu vinavyoweza kufyonzwa na kuvunjwa na mwili.



Opération vaccination COVID-19

Maelezo mapya kuhusu chanjo yanapokatikana, maelezo kwa umma yatarebishwa. Kwa maelezo zaidi, tafadhali rejelea quebec.ca (kwa Kifaransa na Kiingereza). Mwombe mtu akusaidie inayohitajika.

Je, chanjo inafanya kazi katika kupambana na janga?

Chanjo ni moja kati ya mikakati bora zaidi ya kukuinga dhidi ya COVID-19. Inaweza kuzuia ugonjwa au kupunguza matatizo mabaya na kuzuia kifo. Kadri watu wengi wanavyopata chanjo, ndivyo virusi vinavyokuwa na uwezekano mdogo wa kuzalisha. Baada ya muda, vinakufa kama ilivyofanyika kwa magonjwa mengi.

Kwa jumla, chanjo zimedhibiti magonjwa saba mabaya: ndui, dondakoo, pepopunda, homa ya manjano, kifaduro, polio na ukambi.

Je, madhara ya matumizi ya chanjo ya COVID-19 ni gani?

Athari mbaya za chanjo ni kidogo sana ikilinganishwa na madhara mabaya ya COVID-19 yanayoweza kusababisha kifo. Baada ya kupata chanjo, unaweza kuhisi maumivu kwenye sehemu ya sindano. Pia unaweza kushuhudia madhara yafuatayo:

- Uchovu, homa au homa ya baridi
- Maumivu ya kichwa, ya misuli au viungo

Dalili hizi kidogo hadi wastani kwa kawaida hutoweka baada ya siku 1 hadi 2.

Je, chanjo za COVID-19 zinafanya kazi?

Siku kumi na nne hadi 28 baada ya dozi ya kwanza ya chanjo, mtu ana zaidi ya uwezekano wa asilimia 80 kuwa na kingamaradhi ya COVID-19. Dozi ya pili inayopendekezwa imetengenezwa ili kuunda kingamaradhi ya muda mrefu kwa virusi. Kutokana na kiwango cha juu cha kinga baada ya dozi ya kwanza, serikali inapanga kutoa dozi ya pili ndani ya siku 120 (miezi minne).

Je, chanjo za COVID-19 ni salama, hata ingawa zilitengenezwa haraka?

Health Canada imefuata itifaki zilezile madhubuti kama ilivyo kwa chanjo zote. Kutokana na mgogoro unaokabili dunia dhidi ya COVID-19, utafutaji wa chanjo ulikuwa kipaumbele katika nchi zote. Kila hatua inayohitajika ili kutengeneza, kupima na kuthibitisha chanjo ilifanywa kwa ufanisi wa kipekee.

Tangu wakati huo, makumi ya mamiloni ya watu wamepata chanjo duniani kote, bila madhara mabaya na bila vifo vinavyohusiana na chanjo.

Je, ninapaswa kupata chanjo ikiwa nilikuwa na COVID-19?

Hata ikiwa mtu tayari amekuwa na COVID-19, ni muhimu kupata chanjo ya kuongeza kinga. Watu ambao wamekuwa na COVID-19 na wamepata chanjo hawana matukio mengi mabaya.

Je, kwa nini tunahitaji kupata chanjo ikiwa mwili wa binadamu unaweza kushinda COVID-19 kiasili?

Watu wanaopata chanjo dhidi ya COVID-19 wanakingwa dhidi ya ugonjwa huu. Wana uwezekano mdogo wa kuwa na dalili au ugonjwa mabaya.

Je, chanjo ya COVID-19 inaweza kubadilisha DNA yangu?

Hapana. Imani hii inayohusishwa na chanjo za messenger RNA (Pfizer na Moderna) ni uongo. Haiwezekani kabisa kwa chanjo za messenger RNA kubadilisha jeni za mtu. Chanjo haipenyi kiini cha seli ambapo DNA inapatikana. Messenger RNA inadhoofishwa haraka sana na seli.

Je, chanjo za COVID-19 zinafanya kazi dhidi ya virusi vipya?

Ndiyo. Kulingana na data ya hivi punde, chanjo za sasa pia zinafanya kazi dhidi ya virusi vipya nchini Uingereza. Tafiti zinaendelea za virusi vingine kote duniani. Ikihitajika, chanjo zitabadilishwa ili kuweza kukabiliana vizuri na virusi vipya.

Je, kwa nini kuendelea kujikinga baada ya kupata chanjo ya COVID-19?

Hata wakati chanjo imedaiwa kufanya kazi kwa kiwango cha juu, haitoi kinga ya asilimia 100. Mikakati ya afya inaendelea kuhakikisha kuwa unajikinga wewe binafsi na wengine. Itachukua miezi kadhaa kuwapa chanjo watu wengi zaidi.



Kwa maelezo zaidi na kuweka miadi:



Quebec.ca/vaccinCOVID



450 644-4545